# CLASS 6 END TERM 1 AUGUST 2021 KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

____**1**____ huhusisha ukuzaji wa mimea na ____**2**____ wa wanyama. Ni kazi ____**3**____ wengi wetu hudhani kuwa huhusishwa na watu wenye ____**4**____. Pia, wengi ____**5**___ kuwa kazi ya ukulima ni kazi chafu na hatari . Wanafunzi ____**6**_____ shuleni, ni lazima waelekezwe katika mafunzo ____**7**____ na kilimo mapema kwa sababu ____**8**___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Mkulima | B. Kulima | C. Ukulima | D. Mifugo |
| **2.** | A. ufungaji | B. kuwafuga | C. kufungwa | D. ufugaji |
| **3.** | A. ambalo | B. ambayo | C. ambao | D. ambaye |
| **4.** | A. elimu ya chini | B. akili timamu | C. maarifa ya juu | D. elimu ya juu |
| **5.** | A. huchukua | B. huchukulia | C. huchukuliwa | D. huchukia |
| **6.** | A. wanapokuwa | B. wakikuwa | C. wanapokua | D. wakikua |
| **7.** | A. yanayohusu | B. yanahusiana | C. yanayohusiana | D. yanahusu |

**8.** A. mkulima mmoja, walaji wengi
B. haraka haraka haina baraka
C. polepole ndio mwendo
D. chelewa chelewa utapata mwana si wako.

Juzi asubuhi tulipokuwa _____**9**_____, tulisimama wima tukiwa tumetulia kama ____**10**____. Baada ya maskauti ____**11**____ bendera, tuliuimba wimbo wa taifa. Baadaye, mwalimu mkuu alitusabahi, "Hamjambo wanafunzi?" Nasi tukamjibu, "_____**12**____." Alitujibu na ____**13**____ kwa kutupa habari _____**14**_____. Alisema mwalimu wetu wa michezo alikuwa amepata ajali mbaya ya barabarani alipokuwa akiendesha _____**15**____ yake.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. gwarideni | B. uwanjani | C. darasani | D. nyumbani |
| **10.** | A. kondoo | B. simba | C. maji mtungini | D. samaki majini |
| **11.** | A. kushusha | B. kupandisha | C. kushukisha | D. kupaza |

**12.** A. Salama mwalimu, habari yako
B. Nzuri sana, umeamkaje
C. Hatujambo mwalimu, shikamoo
D. Sijambo mwalimu, shikamoo

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **13.** | A. kuanza | B. kumaliza | C. kukamilisha | D. kuendelea |
| **14.** | A. iliyotuchangamsha | B. iliyotuhuzunisha | C. iliyotufurahisha | D. iliyotumaliza |
| **15.** | A. tuktuk | B. meli | C. treni | D. jeti |

***<u>Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.</u>***

**16.** Chagua majina yaliyo katika ngeli ya **I - ZI** pekee.
A. Ndizi, kabati, uzi
B. Meza, kalamu, nyumba
C. Kamba, yai, mdudu
D. Uyoga, pua, shingo

**17.** Ni sentensi gani **haina** kivumishi halisi?
A. Mama alimbeba mtoto mgongoni.
B. Matunda yenyewe ni matamu.
C. Dawa yoyote ya kulevya ni hatari.
D. Madawati mengine yameletwa.

**18.** U hali gani?
A. Salama B. Vyema
C. Njema D. Mzuri

**19.** Kamilisha tashbihi:
**Dada yetu ni mrefu kama**
A. twiga B. korongo
C. mchana D. mlingoti

**20.** Ni sentensi ipi iliyotumia kirejeshi **'amba'** kwa usahihi?
A. Anakula embe ambayo ni mbichi.
B. Darasa ambalo lina wanafunzi ni la sita.
C. Kucheza ambayo alicheza ilipendeza.
D. Kalamu ambacho kinaandika ni changu.

**21.** Ni ala gani ya muziki huchezwa kwa **kupulizwa**?
A. Kinubi B. Gitaa
C. Kayamba D. Tarumbeta

**22.** Chagua sentensi iliyo katika kauli ya **kutendea.**
A. Tuliwapakulia wageni pilau.
B. Mgonjwa amedungwa sindano.
C. Shangazi amefagia chumba.
D. Wavulana wanacheza uwanjani.

**23.** Ni sentensi gani iliyo na mpangilio sahihi wa ***jina, kivumishi, kitenzi*** na ***kielezi***?
A. Mtoto apewe maziwa yake.
B. Ni sharti tuwatunze wanyama.
C. Msichana mwembamba anaimba vizuri.
D. Wanafunzi wote wafunzwe Kiswahili.

**24.** Kamilisha sentensi kwa kiulizi **"ngapi"**
**Mustafa alizawadiwa mara**
A. mangapi?
B. mingapi?
C. wangapi?
D. ngapi?

**25.** Chagua wingi wa sentensi hii:
**Mtoto wangu amemeza dawa.**
A. Watoto wetu wamemeza dawa.
B. Watoto wetu wamemeza madawa.
C. Mtoto wetu amemeza dawa.
D. Mtoto wangu amemeza madawa.

**26.** Mchungwa hutupa machungwa, mpunga hutupa
A. ndizi
B. wali
C. mchele
D. zabibu

**27.** Ni sentensi gani iliyoakifishwa vizuri?
A. Sisi huenda kanisani Jumapili
B. Usipofanya bidii masomoni...
C. Kwa nini mna huzuni!
D. Chezeni polepole, "mama alituambia."

**28.** Kamilisha methali hii:
**Asiyekujua,**
A. siandamane naye.
B. usiku atakuchoma.
C. hakuthamini.
D. marejeo ni ngamani.

**29.** Teua sentensi ambayo haijatumia **'ndi'** kwa usahihi.
A. Hii ndio nguo iliyofuliwa.
B. Wewe ndiwe rafiki yangu.
C. Amina ndiye aliyetuhadithia .
D. Mimi ndimi bingwa wa ushairi.

**30.** Kivumishi cha idadi kimetumika katika sentensi ipi?
A. Madarasa safi huvutia.
B. Mmea wa pili ulikuwa mhindi.
C. Shule yetu ina wanafunzi werevu.
D. Njoo kwangu wakati wowote.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Siku moja ubishi mkali ulizuka miongoni mwa wanyama ambao waliishi katika shamba la Bwana Tindo. Wanyama hao walikuwa ng'ombe, kondoo, kuku, mbwa na paka. Kabla ya ubishi huu, siku zote waliishi kwa amani na upendo. Ubishi wenyewe ulihusu aliyependwa zaidi pale shambani.

Ng'ombe aliamka alipokuwa amejilaza na kuanza maelezo yake. Alieleza kuwa yeye ndiye aliyekuwa bora zaidi kwani alimpa Bwana Tindo maziwa, nyama na ngozi. Aliongeza kuwa maziwa yake humfaa sana mtoto wa mkulima huyo. "Hata baada ya mimi **kuiaga dunia**, mimi huwa na faida kwani ngozi yangu hutumiwa kuundia ngoma, viatu, mavazi, mikanda na mikoba," akamalizia huku akirudi kujilaza.

Kondoo kuona hivyo, alijitetea kwa kusema kuwa yeye ndiye bora zaidi kwani humpa mkulima sufu laini na nyama. "Hata ingawa simpi Bwana Tindo maziwa, yeye hutumia sufu yangu kutengenezea mablanketi mazito yanayomkinga na baridi wakati wa kipupwe," akamalizia.

Kuku aliamka na kuyatikisa manyoya ya mkiani kwa nguvu, kisha akaanza, "Ni nani asiyejua utamu wa nyama yangu? Hakuna mnyama mwenye nyama tamu kuliko mimi. Ni lazima mkulima anipende zaidi yenu kwani hata mayai yangu huwa bora kwa afya yake. Licha ya hayo, sisi huwika na kumwamsha mkulima aanze shughuli za siku," Alijisifu kisha akaketi kwenye tifutifu la vumbi.

Baada ya kuku kumaliza, mbwa aliamka na kueleza kuwa yeye ndiye huwa mlinzi wa pale shambani. Aliongeza kuwa hakuna mnyama aliyeweza kupambana na wezi kama yeye. "Ndio, nyama yangu hailiwi lakini bila mimi, hata nyinyi mngekuwa hatarini. Ni sharti mkulima anipende kuliko nyinyi!" "Sikubaliani nanyi hata kidogo," paka akamkatiza mbwa. "Je, ni nani asiyejua uharibifu wa panya? Ni nani huwanasa na kuwala kama si mimi? Je, hamwoni kuwa mimi ndimi ..." Kabla hajamaliza, Bwana Tindo alitokeza na kuwaambia kuwa, kwa kuwa kila mnyama alikuwa na umuhimu wake, aliwapenda wote. Wakafurahi na kujua kuwa wote walikuwa muhimu na wote walipendwa.

---

**31.** Ubishi uliozuka shambani ulihusu nini?
A. Mnyama aliyekuwa mzuri zaidi.
B. Yule aliyependwa kuliko wote.
C. Yule aliyependeza mno.
D. Mnyama mwenye faida nyingi.

**32.** Kitambo kabla ya siku ya ubishi, wanyama hao waliishi
A. wakizozana B. kwa amani
C. wakipendeza D. wakiaminiana

**33.** Chagua orodha ya wanyama waliotajwa katika kifungu.
A. Kuku, sungura, mbwa, paka na ng'ombe.
B. Ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na mbwa.
C. Mbwa, paka, punda, ng'ombe na kondoo.
D. Kondoo, paka, ng'ombe, kuku na mbwa.

**34.** Kulingana na ufahamu, afya bora ya mwana wa Tindo ilimtegemea sana
A. ng'ombe B. mbwa
C. kondoo D. paka

**35.** Kifungu **kuiaga dunia** kama kilivyotumika katika aya ya pili ni aina ya
A. kufa
B. nahau
C. kuacha watu
D. tashbihi

**36.** Taarifa inasema kuwa kuku
A. ni mlinzi hodari wa shambani.
B. hutoa sufu laini ajabu.
C. ana nyama tamu kuliko wote.
D. hupambana vilivyo na panya.

**37.** Unadhani ni wanyama wangapi ambao Bwana Tindo aliwategemea kwa nyama?
A. Watatu
B. Ng'ombe, kondoo, na kuku
C. Watano
D. mbwa na paka

**38.** Ili mkulima arauke, alimtegemea
A. paka B. ng'ombe
C. mbwa D. kuku

**39.** Wanyama ambao hawakumaliza maelezo yao walikuwa
A. paka na mbwa
B. ng'ombe na paka
C. paka na kuku
D. mbwa na kondoo

**40.** Kwa maoni yako, ni mnyama yupi aliyekuwa muhimu zaidi?
A. Ng'ombe
B. Wote
C. Kuku
D. Kondoo

***So… …ungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Ni jambo la kutia moyo sana kuona jinsi ambavyo viwango vya ajali za barabarani vimepungua. Kitambo, ungesikia visa vingi mno vya ajali barabarani zikitangazwa kwenye runinga, redio n hata magazetini. Wakati huo, watu wengi hasa wanaoishi mijini waliogopa sana kusafiri wasije wakapoteza maisha yao.

Kinyume na hapo awali, madereva sasa wamepunguza tabia ya **kupiga maji** na wengine kuacha kabisa. Hali hii ya ulevi ilikuwa ikichangia mno ajali za barabarani kwa sababu, madereva wakiwa walevi, wao hupoteza uzingativu wanapoendesha magari. Ni ukweli pia kusema kuwa siku hizi hakuna **madereva bandia** wasio na vyeti vya udereva. Hatua hii imewarahisishia kazi maafisa wa trafiki ambao kitambo hawakuwa na imani na madereva wengine.

Barabara nyingi na mijini sasa zinaangaziwa kwa kamera za siri mchana kutwa na usiku kucha. Hali hii imepunguza ufisadi ambapo baadhi ya maafisa wa trafiki walikuwa wakipokea hongo waziwazi kutoka kwa madereva na makondakta wanaovunja sheria za barabarani. Licha ya hayo, alama na ishara za barabarani sana zimewekwa upya na kwa rangi za kuyanasa macho kwa haraka zaidi. Hata madereva "vipofu" sasa wanaweza kuziona.

Waendao kwa miguu nao wamechangia kwa kuzingatia ufuasi wa sheria. Siku hizi, waendao kwa miguu hawavukii barabara popote bali kwenye **sehemu spesheli** iliyotengwa kwa kuvukia barabara. Wengi wao sasa wamepunguza haraka walizokuwa nazo kwa kuamini kuwa haraka haraka haina baraka.

Serikali inastahili kuongeza bidii ili kuvipunguza zaidi au hata kuvimaliza visa vya ajali za barabarani. Hili litawezekana ikiwa maafisa wa trafiki wataongezwa mishahara ili wasiwe na tamaa ya kuchukua hongo, barabara zaidi zitajengwa na zile zilizopo kuboreshwa zaidi na kuhakikisha kuwa magari mabovu hayaruhusiwi kuhudumu barabarani. Hali ikiwa hivi, tutafurahia usafiri.

**41.** Inafurahisha kuwa
A. ajali zimepungua nchini.
B. madereva wamekuwa wema.
C. barabara zina kamera za siri.
D. serikali imechangia kupunguza ajali.

**42.** Kulingana na paragrafu ya kwanza, visa vya ajali havikutangazwa katika
A. redio  B. runinga
C. magazeti  D. majarida

**43.** Zamani, watu wanaoishi mijini waliogopa kusafiri kwa sababu
A. ajali zilikuwa nyingi.
B. hawakutaka kufa.
C. barabara zilikuwa mbovu.
D. madereva walikuwa walevi.

**44.** **Kupiga maji** ni sawa na
A. kutumia dawa za kulevya.
B. kuvuta sigara.
C. kunywa pombe.
D. kuwa mlevi.

**45.** **Madereva bandia** ni wale ambao
A. hupiga maji.
B. hulewa kupindukia.
C. huendesha magari.
D. hawana vyeti vya uendeshaji.

**46.** Kamera za siri zimechangia vipi kupunguza viwango vya ajali?
A. Huangazia matukio ya barabarani.
B. Huonekana na hata madereva "vipofu"
C. Vinawatambulisha madereva bandia.
D. Vinasaidia kushiriki hongo.

**47.** Taarifa hii imetumia methali ngapi?
A. 2  B. 3
C. 1  D. 4

**48.** Kulingana na ufahamu huu, **sehemu spesheli** ni
A. barabarani
B. kwenye matuta
C. kando kando ya barabara.
D. kwenye kivukomilia.

**49.** Katika aya ya mwisho, mwandishi anaishauri serikali kufanya mambo mangapi?
A. Manne  B. Mawili
C. Matatu  D. Matano

**50.** Taarifa hii inafaa mada gani?
A. Ajali za barabarani
B. Kupungua kwa ajali za barabarani
C. Ajali
D. Barabara zetu

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com